JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI MHESHIMIWA MUSTAFA HAIDI MKULO(MB) AKIJIBU HOJA ZA WABUNGE KUHUSU TAARIFA YA HALI YA UCHUMI MWAKA 2009 NA HOTUBA YA BAJETI YA SERIKALI 2010/11

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

DODOMA

JUNI, 2010

MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI

MHESHIMIWA MUSTAFA HAIDI MKULO (MB)

AKIJIBU HOJA ZA WABUNGE KUHUSU TAARIFA YA HALI YA UCHUMI MWAKA 2009 NA HOTUBA YA BAJETI YA SERIKALI 2010/11

1. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, na Naibu Spika kwa kuongoza vyema mjadala wa Hotuba kuhusu Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2009 na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2010/11.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nieleze kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge yatasaidia sana katika utekelezaji wa bajeti mwakani. Nawashukuru wote.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba zangu mbili zimechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 64 waliochangia kwa kuzungumza. Napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kama ifuatavyo:

1. Mhe. Dkt. Abdallah Omari Kigoda (Mb.)-Handeni
2. Mhe. Hamad Rashid Mohamed (Mb.)-Wawi
3. Mhe. Athumani Said Janguo (Mb – Kisarawe)
4. Mhe. Juma Hassan Kilimbah (Mb – Iramba Magharibi)
5. Mhe. Mgana Izumbe Msindai (Mb – Iramba Mashariki)

6. Mhe. Dkt. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya (Mb – Kwela)
7. Mhe. Kabwe Zuberi Zitto (Mb – Kigoma Kaskazini)
8. Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura (Mb – Tunduru)
9. Mhe. Khadija Salum Ally Al-Qassmy (Mb – Viti Maalum)
10. Mhe. Ahmed Ally Salum (Mb - Solwa)
11. Mhe. Siraju Juma Kaboyonga (Mb - Tabora Mjini)
12. Mhe. Balozi Dkt. Getrude Ibengwe Mongella(Mb - Ukerewe)
13. Mhe. Herbert James Mntangi (Mb - Muheza)
14. Mhe. Esther Kabaki Nyawazwa (Mb – Viti Maalum)
15. Mhe. Ruth Blasio Msafiri (Mb – Muleba Kaskazini)
16. Mhe. Raynald Alfons Mrope (Mb – Masasi)
17. Mhe. Mussa Azan Zungu (Mb – Ilala)
18. Mhe. Ali Khamis Seif (Mb – Mkoani)
19. Mhe. Balozi Abdi Hassan Mshangama (Mb – Lushoto)
20. Mhe. Shoka Khamis Juma (Mb – Micheweni)
21. Mhe. Damas Pascal Nakei (Mb – Babati Vijijini)
22. Mhe. Kidawa Hamis Saleh (Mb – Viti Maalum)
23. Mhe. Prof. Idris Ali Mtulia (Mb – Rufiji)
24. Mhe. Salim Yussuf Mohamed (Mb – Kojani)
25. Mhe. John Momose Cheyo (Mb – Bariadi Mashariki)
26. Mhe. Dunstan Daniel Mkapa (Mb – Nanyumbu)
27. Mhe. Dkt. Juma Alifa Ngasongwa (Mb – Ulanga Magharibi)
28. Mhe. Eng. Muhammed Habib Juma Mnyaa (Mb – Mkanyageni)
29. Mhe. Ania Said Chaurembo (Mb – Viti Maalum)
30. Mhe. Charles N. Keenja (Mb – Ubungo)

31. Mhe. Nuru Awadhi Bafadhil (Mb – Viti Maalum)
32. Mhe. Said Amour Arfi (Mb - Mpanda Kati)
33. Mhe. Suleiman Omar Kumchaya (Mb – Lulindi)
34. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma (Mb – Viti Maalum)
35. Mhe. Kilontsi M. Mporogomyi (Mb – Kasulu Magharibi)
36. Mhe. Manju Salum Omar Msambya (Mb – Kigoma Kusini)
37. Mhe. Salim Hemed Khamis (Mb – Chambani)
38. Mhe. Dkt. Omari Mzeru Nibuka (Mb – Morogoro Mjini)
39. Mhe. Lucy Thomas Mayenga (Mb – Viti Maalum)
40. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa (Mb – Biharamulo Magharibi)
41. Mhe. Wilson Mutaganywa Masilingi (Mb – Muleba Kusini)
42. Mhe. Thomas Abson Mwang'onda (Mb – Kuteuliwa)
43. Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe (Mb – Kyela)
44. Mhe. Joseph James Mungai (Mb – Mufindi Kaskazini)
45. Mhe. Ibrahim Muhammad Sanya (Mb – Mji Mkongwe)
46. Mhe. Maria Ibeshi Hewa (Mb – Viti Maalum)
47. Mhe. Mwadini Abbas Jecha (Mb – Wete)
48. Mhe. Elizabeth Nkunga Batenga (Mb – Viti Maalum)
49. Mhe. Mariam Salum Mfaki (Mb – Viti Maalum)
50. Mhe. Basil Pesambili Mramba (Mb – Rombo)
51. Mhe. Dkt. Anthony Mwandu Diallo (Mb – Ilemela)
52. Mhe. Suzan Anselm Jerome Lyimo (Mb – Viti Maalum)
53. Mhe. George B. Simbachawene (Mb – Kibakwe)
54. Mhe. Cynthia Hilda Ngoye (Mb – Viti Maalum)
55. Mhe. Eng. Stela Martin Manyanya (Mb – Viti Maalum)

56. Mhe. Mary Michael Nagu (Mb) –Waziri: Viwanda, Biashara na Masoko
57. Mhe. Capt. John Zefania Chiligati (Mb): Waziri-Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
58. Mhe. Stephen Masatu Wasira (Mb) – Waziri: Kilimo, Chakula na Ushirika
59. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Magembe (Mb) – Waziri: Elimu na Mafunzo ya Ufundi
60. Mhe. Aisha Omar Kigoda (Mb) – Naibu Waziri: Afya na Ustawi wa Jamii
61. Mhe. William Mganga Ngeleja (Mb) – Waziri: Nishati na Madini
62. Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa (Mb) – Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu
63. Mhe. Shamsa Selengia Mwangunga (Mb) – Waziri:Maliasili na Utalii
64. Mhe. Omar Yusuf Mzee (Mb.) Naibu Waziri: Fedha na Uchumi

4. ***Mheshimiwa Spika,*** Waheshimiwa Wabunge 83 wamechangia kwa maandishi, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Omari Shabani Kwaangw' (Mb – Babati Mjini)
2. Mhe. Balozi Abdi Hassan Mshangama (Mb – Lushoto)
3. Mhe. Eustace Osler Katagira (Mb – Kyerwa)
4. Mhe. Mgana Izumbe Msindai (Mb – Iramba Mashariki)
5. Mhe. Daniel Nicodem Nsanzugwanko (Mb– Kasulu Mashariki)
6. Mhe. Mwadini Abbas Jecha (Mb – Wete)

7. Mhe. Margareth Agnes Mkanga (Mb – Viti Maalum)
8. Mhe. Hemed Mohamed Hemed (Mb – Chonga)
9. Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa (Mb - Lupa)
10. Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni (Mb – Busega)
11. Mhe. Godfrey Weston Zambi (Mb – Mbozi Mashariki)
12. Mhe. Lucy Fidelis Owenya (Mb – Viti Maalum)
13. Mhe. Prof. Philemon Mikol Sarungi (Mb – Rorya)
14. Mhe. Mhonga Said Ruhwanya (Mb – Viti Maalum)
15. Mhe. Maua Abeid Daftari (Mb – Viti Maalum)
16. Mhe. Mwinchoum Abdulrahman Msomi (Mb – Kigamboni)
17. Mhe. Halima Omar Kimbau (Mb – Viti Maalum)
18. Mhe. Kabwe Zuberi Zitto (Mb – Kigoma Kaskazini)
19. Mhe. Diana Mkumbo Chilolo (Mb – Viti Maalum)
20. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb – Viti Maalum)
21. Mhe. Meryce Mussa Emmanuel (Mb – Viti Maalum)
22. Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga (Mb – Viti Maalum)
23. Mhe. Mgeni Jadi Kadika (Mb – Viti Maalum)
24. Mhe. Janeth Mourice Massaburi (Mb – Viti Maalum)
25. Mhe. Castor Raphael Ligallama (Mb – Kilombero)
26. Mhe. Mohammed Rajab Soud (Mb – Jang'ombe)
27. Mhe. Prof. Raphael Benedict Mwalyosi (Mb – Ludewa)
28. Mhe. Magdalena Hamis Sakaya (Mb – Viti Maalum)
29. Mhe. Masoud Abdallah Salim (Mb – Mtambile)
30. Mhe. Masolwa Cosmas Masolwa (Mb – Bububu)
31. Mhe. Margaret Simwanza Sitta (Mb – Viti Maalum)

32. Mhe. Omar Ali Mzee (Mb – Ziwani)
33. Mhe. Nuru Awadhi Bafadhil (Mb – Viti Maalum)
34. Mhe. Riziki Omar Juma (Mb – Viti Maalum)
35. Mhe. Mudhihir Mohamed Mudhihir (Mb – Mchinga)
36. Mhe. Juma Abdallah Njwayo (Mb – Tandahimba)
37. Mhe. Samuel Mchele Chitalilo (Mb – Buchosa)
38. Mhe. Siraju Juma Kaboyonga (Mb – Tabora Mjini)
39. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu (Mb – Viti Maalum)
40. Mhe. Bujiku Philip Sakila (Mb – Kwimba)
41. Mhe. John Paul Lwanji (Mb – Manyoni Magharibi)
42. Mhe. Paul Peter Kimiti (Mb – Sumbawanga Mjini)
43. Mhe. Juma Hassan Kilimbah (Mb – Iramba Magharibi)
44. Mhe. Mohamed Abdi Abdulaziz (Mb – Lindi Mjini)
45. Mhe. Capt. John Zefania Chiligati (Mb – Manyoni Mashariki)
46. Mhe. Mwaka Abdulrahaman Ramadhan (Mb – Viti Maalum)
47. Mhe. Nazir Mustafa Karamagi (Mb – Bukoba Vijijini)
48. Mhe. Ali Juma Haji (Mb – Chaani)
49. Mhe. Ruth Blasio Msafiri (Mb – Muleba Kaskazini)
50. Mhe. Benedict Ngalama Ole-Nangoro (Mb – Kiteto)
51. Mhe. Prof. Raphael Benedict Mwalyosi (Mb – Ludewa)
52. Mhe. Dkt. Cyril August Chami (Mb – Moshi Vijijini)
53. Mhe. Juma Said Omar (Mb – Mtabwe)
54. Mhe. Michael Lekule Laizer (Mb - Longido)
55. Mhe. Harith Bakari Mwapachu (Mb – Tanga)
56. Mhe. Mariam Reuben Kasembe (Mb – Viti Maalum)

57. Mhe. Dkt. Luka Jelas Siyame (Mb – Mbozi Magharibi)
58. Mhe. Damas Pascal Nakei (Mb – Babati Vijijini)
59. Mhe. Yono Stanley Kevela (Mb – Njombe Magharibi)
60. Mhe. Florence Essa Kyendesya (Mb – Viti Maalum)
61. Mhe. Zaynab Matitu Vulu (Mb – Viti Maalum)
62. Mhe. Mbaruk Kassim Mwandoro (Mb – Mkinga)
63. Mhe. Lolesia J.M Bukwimba (Mb – Busanda)
64. Mhe. Bakari Shamis Faki (Mb – Ole)
65. Mhe. Charles Muguta Kajege (Mb – Mwibara)
66. Mhe. Eng. Mohamed Habib Juma Mnyaa (Mb – Mkanyageni)
67. Mhe. Teddy Louise Kasella-Bantu (Mb – Bukene)
68. Mhe. Vuai Abdalah Khamis (Mb – Magogoni)
69. Mhe. Eng. Laus Omar Mhina (Mb – Korogwe Vijijini)
70. Mhe. Zubeir Ali Maulid (Mb – Kwamtipura)
71. Mhe. Dkt. Omari Mzeru Nibuka (Mb – Morogoro Mjini)
72. Mhe. Maida Hamad Abdallah (Mb – Viti Maalum)
73. Mhe. Dkt. James Mnanka Wanyancha (Mb – Serengeti)
74. Mhe. Khadija Saleh Ngozi (Mb – Kuteuliwa)
75. Mhe. Dkt. Charles Ogesa Mlingwa (Mb – Shinyanga Mjini)
76. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya (Mb – Viti Maalum)
77. Mhe. Mwantumu Bakari Mahiza (Mb – Viti Maalum)
78. Mhe. Aloyce Bent Kimaro (Mb – Vunjo)
79. Mhe. Anastazia James Wambura (Mb – Viti Maalum)
80. Mhe. Devota Mkuwa Likokola (Mb – Viti Maalum)
81. Mhe. John Momose Cheyo (Mb – Bariadi Mashariki)

82. Mhe. Mhe. Charles N. Keenja (Mb – Ubungo)

83. Mhe. Andrew John Chenge (Mb – Bariadi Magharibi)

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, nafarijika kwa michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nitaeleza kwa muhtasari majibu kwa hoja zilizotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Kamati ya Fedha na Uchumi

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Fedha na Uchumi imetoa mapendekezo mazuri ambayo Serikali imeyakubali na inaahidi kuyafanyia kazi. Baadhi ya mapendekezo hayo ni kupanua wigo wa kuongeza mapato, kuangalia eneo la sera na uendeshaji wa taratibu za kukusanya kodi, kuimarisha Mpango Mkakati wa TRA wa kuboresha ukusanyaji kodi, kuangalia upya utaratibu wa kuanzisha Mamlaka na Wakala za Serikali ambao sasa vinainyima Serikali mapato.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu misamaha ya kodi katika tasnia ya madini, Serikali imeingia mikataba na Kampuni za madini (Mining Development Agreements) ambayo imeainisha vivutio vya kodi. Aidha, kila kampuni ina mkataba wake tofauti na Serikali. Katika hotuba yangu ya Bajeti, nimefafanua kwamba Serikali itatoa unafuu maalum wa Kodi ya

Ongezeko la Thamani na msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa za petroli kwa kampuni zilizosaini mikataba na Serikali. Msamaha utatolewa kulingana na masharti yaliyopo kwenye mikataba iliyosainiwa kati ya Serikali na kampuni za madini kabla ya Julai, 1, 2009. Kwa mantiki hiyo, kampuni zote ambazo ziliingia mikataba baada ya Julai, 1, 2009 na ambazo hazina mikataba hazihusiki na msamaha huo. Kwa kuwa mikataba ya kabla ya Julai 2009 iliingiwa kati ya Serikali na kampuni hizo, ni vigumu kisheria kwa Serikali kuamua yenyewe kufanya marekebisho ya vivutio vya kodi kwa lengo la kuzipunguzia bila kuzihusisha kampuni husika. Serikali itaendelea na mazungumzo na kampuni za madini ili kurejea mikataba hiyo kwa lengo la kuweka uwiano sawa katika kugawana mapato yanayotokana na rasilimali ya madini. Kazi hii ilishaanza kwa baadhi ya kampuni na mwelekeo ni wa kuridhisha.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa matumizi, Kamati imesisitiza umuhimu wa Serikali kuainisha matumizi yake na uwezo wa kuamsha mapato. Serikali ichunguze matumizi yake na kuhakikisha kuwa ni ya kimkakati. Aidha, Kamati imeshauri Serikali ije na mkakati wa makusudi wa kupunguza matumizi yake yasiyo ya lazima (cost cutting measures).

9. ***Mheshimiwa Spika,*** wakati nawasilisha hotuba ya bajeti ya 2010/11 nilielezea hatua mbalimbali zitazochukuliwa na Serikali kupunguza matumizi. Hatua hizo ni pamoja na:

(i) Kudhibiti matumizi ya simu na umeme:

(ii) Kudhibiti Matumizi ya Magari:

(iii) Kuhakikisha kwamba, Serikali inalipa posho za nyumba kutokana na uwezo wa bajeti.

(iv) Fedha zilizopangwa kwa ajili ya posho mbalimbali katika Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri zitapunguzwa na kudhibitiwa;

(v) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani juu ya uandaaji wa hesabu katika viwango vya kimataifa (IPSAS);

(vi) Kuanzia mwaka 2010/11, Halmashauri zinatakiwa kuonesha bakaa katika akaunti ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha ili zijumuishwe kwenye bajeti ya mwaka unaofuata kama chanzo cha mapato;

(vii) Serikali itatumia utaratibu wa malipo unaosimamiwa na Benki Kuu (Tanzania Interbank Settlement System - TISS) kwa malipo yatakayofanywa na Wizara zote zilizopo Dar es salaam na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;

(viii) Kudhibiti utoaji wa dhamana za Serikali kwa vyombo mbalimbali vya umma ili kuepuka ongezeko lisilohimilika la deni la Taifa; na

(ix) Serikali itakuwa na chombo maalum kitakachosimamia ujenzi na viwango vya majengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Bajeti ya mwaka 2010/11 itatekelezwa kwa kuzingatia malengo yaliyokusudiwa na kuleta tija.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mikopo ya kibiashara, ningependa kufafanua kwamba Serikali inategemea kukopa mikopo ya kibiashara ya kiasi cha shilingi 1331.2 bilioni kutoka ndani na nje ya nchi. Bado mikopo ya kibiashara itazingatia masharti nafuu ikiwa ni pamoja na muda wa kurejesha mikopo usiopungua miaka mitano na zaidi pamoja na riba nafuu. Mikopo ya ndani itatokana na uuzaji wa hatifungani za Serikali za muda mrefu. Aidha, Serikali itahakikisha mikopo hiyo haiathiri hali ya utulivu wa kiuchumi na kutokuikosesha sekta binafsi mikopo ya riba nafuu. Tumekuwa tukikopa mikopo ya ndani yenye masharti ya namna hii hadi sasa kwa hiyo siyo jambo geni. Vile vile, napenda kusisitiza kwamba mikopo hii itatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Sababu za Serikali kuanza kukopa mikopo ya kibiashara kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni upungufu wa mapato ya ndani na mikopo na misaada ya wahisani katika kuongeza kasi ya utekelezaji MKUKUTA na dira ya maendeleo 2025 hasa katika maeneo ya miundombinu (barabara, reli, nishati, maji, bandari na madaraja), kilimo hasa cha umwagiliaji na viwanda vya msingi. Ni muhimu

kuongeza kasi ya kuwekeza katika maeneo haya ili kuwezesha uchumi kukua kwa haraka zaidi na hivyo kuongeza kasi ya kupunguza umasikini nchini. Kutumia mikopo kibiashara kwa miradi ya maendeleo ni utaratibu unaokubalika.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, Kamati imeishauri Serikali kupunguza urasimu na kuharakisha mchakato wa utoaji maamuzi, kuboresha utoaji wa utaratibu wa utoaji leseni na kuwa na mfumo wa kodi unaovutia uwekezaji. Serikali imekubaliana na ushauri huu na hatua za kufanikisha hili zitaendelea kuchukuliwa. Aidha, katika hotuba yangu nilipowasilisha taarifa ya hali ya uchumi, baadhi ya hatua katika eneo hili nilizielezea.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, Kamati imetoa mapendekezo mengi ambayo Serikali imeyakubali na itaendelea kuyafanyia kazi. Nachukua fursa hii kuishukuru tena Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya 2010/11.

Kambi ya Upinzani

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Kambi ya Upinzani imetoa ushauri na mapendekezo mengi ikiwa ni pamoja na bajeti mbadala. Mapendekezo hayo ni pamoja na kuitaka Serikali kuziwezesha asasi ndogo ndogo za fedha kupata mikopo nafuu au kuingia nazo ubia ili kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwa riba nafuu inayolipika, kuhakikisha kwamba nchi

ina umeme wa uhakika, Serikali kutumia teknolojia ya *mapping* ili kujua rasilimali zote zilizopo nchini na namna tunavyoweza kuzitumia, kuzipa uwezo wa kujiendesha NDC na STAMICO ili ziweze kumiliki maeneo ya *Industrial Minerals* na kuingia ubia na makampuni ya nje bila kudhulumiwa na Serikali iendelee kupima ardhi ili kuwezesha wananchi kumiliki ardhi hasa kutokana na nchi kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali inayaafiki mapendekezo hayo na itaendelea kuyafanyia kazi.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na ushauri uliotolewa kambi ya upinzani pia imetoa Bajeti mbadala kwa Serikali kuichambua. Serikali imeiangalia Bajeti mbadala na kubaini kuwa mapendekezo mengi ni mazuri. Hata hivyo Serikali inashauri kwamba katika suala la vianzo vya mapato ni vyema kwa miaka ijayo mapendekezo haya yakawasilishwa Serikalini mapema ili yajumuishwe katika mchakato wa bajeti. Kwa kawaida mchakato wa Bajeti huanza mwezi Novemba na kumalizika mwezi Februari ili kuhakikisha kuwa maamuzi muhimu yanachukuliwa kati ya mwezi Machi na Mei. Kama mapendekezo yaliyopo katika Bajeti mbadala yangewasilishwa mapema wataalam wangeyachambua kwa kina na nina hakika yangeweza kujumuishwa katika Bajeti ya mwaka 2010/11.

15. ***Mheshimiwa*** **Spika,** kutokana na msukosuko wa fedha na uchumi duniani, serikali iliandaa mpango wa kuunusuru uchumi na athari za msukosuko (Rescue Package). Mpango wa dharura wa muda mfupi uliandaliwa na gharama zake zilikadiriwa kufikia shilingi 1.7 trillion. Serikali ilitarajia kupata fedha hizi kutoka vyanzo mbali ikiwa pamoja na wafadhili

na kukopa kutoka masoko ya ndani. Mheshimiwa Spika, hadi sasa shilingi trilioni 1.298 zimekwishapatikana, na zimetumika kama ifuatavyo:-

(a) Kuziba pengo la bajeti lililotokana na upungufu wa mapato ya ndani;

Jumla ya shilingi 766.3 bilioni zilikopwa kupitia dhamana za serikali ikilinganishwa na shilingi 828 bilioni zilizotarajiwa.

(b) Kuziba pengo la akiba ya fedha za kigeni;

Benki kuu imeshapokea kiasi cha shilingi 411.2 bilioni kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) chini ya utaratibu wa Exogenous Shock Facility (ESF) ukilinganisha na shilingi 436.2 bilioni zilizotarajiwa ili kuongeza akiba ya fedha kigeni.

(c) Kulinda ajira na vipato;

Kiasi cha shilingi 19.2 billion kimeshalipwa kama fidia ya hasara (loss compensation) kwa makampuni na wafanyabiashara binafsi waliopata hasara ya moja kwa moja kutokana na kuporomoka kwa bei za kahawa na pamba ukilinganisha na shilingi 21.9 bilioni zilizokadiriwa. Kwa upande mwingine jumla ya shilingi 15 bilioni zimetengwa kwa ajili ya kudhamini mikopo (loan rescheduling with Government guarantee) kwa makampuni na wafanya biashara binafsi wa sekta mbali mbali walioshindwa kurudisha mikopo yao kwa wakati uliotakiwa kutokana na kushindwa kufikia malengo ya mapato. Chini ya

mpango huu, shilingi 45 bilioni zilikadiriwa kutumika. Lengo la hatua hizi ni kuwawezesha wakopaji kupata mikopo mipya kwa ajili ya shughuli za ununuzi wa mazao kwa msimu wa 2009/2010. Vile vile kiasi cha shilingi 20 bilioni zilitolewa chini ya mpango huo ikiwa ni ruzuku kwa bei ya zao la pamba. Serikali pia ilitoa kiasi cha shilingi 8 bilioni kwa lengo la kupanua mifuko ya dhamana ya ECGS na SMEs.

(d) Kuhakikisha usalama wa chakula

Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 10 bilioni ili kuongeza akiba ya chakula kwa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Chakula (NFRA). Aidha serikali imeshatoa shilingi 20 bilioni kwa ajili ya mikopo ya pembejeo za kilimo na benki ya rasilimali (TIB) imeshapokea kiasi cha shilingi 19 bilioni kwa ajili ya kuiwezesha kutoa mikopo ya kilimo.

(e) Kulinda uwekezaji muhimu hususan miundombinu

Serikali imeshatoa kiasi cha shilingi 10 bilioni kama mikopo kupitia Benki ya Rasilimali (TIB) kwa ajili ya kugharamia uwekezaji katika sekta ya nishati ukanda wa kusini.

Hivyo, basi fedha zote zilizopatikana zimetumika kama ilivyoainishwa hapo juu. Serikali bado inaendelea na juhudi za kutafuta kiasi cha takriban shilingi 400 bilioni zinazohitajika ili kuukamilisha mpango wote. Hata hivyo,

matumizi katika baadhi ya vifungu, yatapungua ukiinganisha na mpango wa awali. Mafungu makubwa ni kama:

(a) Mikopo ya masharti nafuu:
Serikali ilitarajia kutumia kiasi cha shilingi bilioni 80. Kiasi hiki hakitahitajika tena kwa sababu Serikali ilikitoa.

(b) Kusaidia Shirika la Reli (TRL)
Kiasi cha Shilingi 110.4 bilioni kingehitajika. Kiasi hiki hakitahitajika tena baada ya mkataba baina ya Serikali na TRL kusitishwa.

(c) Dhamana kwa Mikopo
Kiasi cha shilingi 30 bilioni hazitatumika kwa sababu mikopo iliyokidhi masharti ilihitaji kiasi cha shilingi 15 bilioni tu.

Serikali inaandaa taarifa kamili ya utekelezaji wa mpango mzima na mara taarifa itakapokamilika itakuwa ndiyo msingi wa ukaguzi wa fedha hizo.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi na ule wa Kambi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge waliotoa, michango yao ya maoni na ushauri utasaidia katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2010/11. Baadhi ya mapendekezo yalihusisha maeneo yafuatayo: kupunguza riba za kukopa na kuongeza riba za amana, vyanzo

vipya vya mapato, kuimarisha miundombinu ya reli na barabara, kuboresha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuboresha sekta za jamii, mgawanyo wa mapato ya muungano, kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi waliopo pembezoni mwa nchi, kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima, kurahisisha masharti ya dirisha la kilimo la TIB, kuimarisha sarafu ya nchi yetu, kuongeza fursa za ajira, kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya uchaguzi mkuu, kuhakikisha Serikali inafanya tathmini na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru uchumi na Serikali kupunguza utegemezi kwa misaada kutoka nje. Tumechukua ushauri huu na tutaufanyia kazi.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kujibu baadhi ya hoja hizo kama ifuatavyo, kuhusu riba za mabenki kulingana na Sheria ya Mabenki na Vyombo vya Fedha ya mwaka 1991, pamoja na ile iliyorekebishwa mwaka 2006. Benki za biashara zimeruhusiwa kupanga riba kulingana na ushindani katika soko. Kwa hiyo, katika kupanga viwango vya riba, benki za biashara huzingatia ushindani katika soko la fedha na mitaji, gharama za upatikanaji wa fedha, gharama za uendeshaji na sifa za mkopaji.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kiwango kikubwa, riba hutegemea sifa alizonazo mkopaji. Kukosekana kwa taarifa sahihi za wakopaji na kutokuwepo kwa taasisi ya kuhakiki ukweli wa taarifa za waombaji mikopo (Credit Reference Bureau) nchini, vimechangia kwa kiasi kikubwa kufanya viwango vya riba za mikopo kuwa juu. Mchakato wa kuanzisha vyombo vya

kuhifadhia taarifa za wakopaji umekwishaanza na upo katika hatua nzuri. Kuwepo kwa vitambulisho vya taifa pia kutasaidia kupunguza tatizo hili.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu maeneo mapya ya kutoza kodi hasa maduka ya fedha za kigeni, Saloon na migahawa ni kwamba: kulingana na sheria za kodi zilizopo, biashara za maduka ya fedha za Kigeni, Saloon na Migahawa hutozwa kodi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kodi ya Mapato na Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hata hivyo, Kodi ya Ongezeko la Thamani inatozwa kwa biashara ya migahawa na Saloon kama biashara husika imefikia kiwango cha usajili wa VAT ambacho ni shilingi 40 milioni kwa mwaka.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa kuboresha sekta ndogo ya uvuvi kuondoa kodi kwenye vipuri na injini napenda nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba injini na nyavu za uvuvi tayari zimesamehewa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Aidha, injini za boti za uvuvi na nyuzi za kutengenezea nyavu za uvuvi hazitozwi ushuru wa forodha.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa kugawana mapato kutokana na vyanzo vya muungano nasema kuwa mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha (Joint Finance Commission) kuhusu Vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za uendeshaji wa shughuli za muungano yamekuwa yakifanyiwa kazi na Serikali zetu mbili, ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kila upande umeshaandaa mapendekezo yake ambayo yamepangwa kujadiliwa kwenye vikao vya pamoja chini ya

Uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuvuta subira kwani masuala haya yanahitaji mashauriano ya pamoja.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa kuboresha mazingira ya kazi ya maeneo ya pembezoni, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ili kuwavutia watumishi katika maeneo hayo. Kwa mwaka 2010/11, Serikali imetenga jumla ya shilingi 66.85 bilioni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi (maboma ya Halmashauri), nyumba za Watumishi, Zahanati na vituo vya afya, miradi ya maji, madaraja vijijini, hosteli za wanafunzi wa kike katika shule za sekondari, na ununuzi wa boti na magari. Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kufanikisha azma hii.

23. ***Mheshimiwa Spika***, Katika miezi ya hivi karibuni, thamani ya shilingi ya kitanzania dhidi ya dola ya kimarekani imekuwa ikipungua. Kwa kipindi cha mwaka ulioishia Aprili 2010, shilingi ya kitanzania ilipoteza thamani dhidi ya dola ya kimarekani kwa asilimia 1.2. Kupungua huku kwa thamani kumetokana na kuimarika kwa dola ya kimarekani, kufuatia kuzorota kwa sarafu ya euro.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** hivi sasa, wawekezaji wanaiona dola ya kimarekani kama sarafu iliyo bora zaidi duniani, hasa katika kipindi hiki ambacho nchi za Ulaya zinajaribu kujikwamua na tatizo la madeni sugu ya nchi ya Ugiriki, ambayo yamesababisha sarafu za Ulaya hususan euro, kuanguka. Hata sarafu ambazo zimekuwa na historia ya uimara kama dola

za Australia na Canada zimeanguka dhidi ya dola ya kimarekani. Hapa Afrika Mashariki, kati ya tarehe 6 na 20 Machi 2010, wakati shilingi ya Tanzania imeanguka kwa asilimia 0.7 tu, shilingi ya Kenya imeanguka kwa kiasi cha asilimia 1.3 na ya Uganda imeanguka kwa asilimia 2.5.

Sababu ya pili ni ongezeko la manunuzi ya dola na mabenki hapa nchini kwa ajili ya kuongeza akiba zao za fedha za kigeni. Ongezeko hili limetokana na kupungua kwa kasi ya utoaji mikopo kutoka mabenki, kufuatia msukosuko wa uchumi duniani. Katika kipindi hiki, mabenki yamekuwa makini zaidi katika kutoa mikopo na hivyo kuongeza zaidi uwekaji wa akiba katika rasilimali za fedha za kigeni badala ya kutoa mikopo.

25. ***Mheshimiwa Spika*** kuhusu hoja kuwa kushuka kwa thamani ya shilingi, kunazorotesha uchumi, ni kwamba, kwa upande mmoja, kupungua kwa thamani ya shilingi kunaongeza bei ya bidhaa tunazoagiza toka nje, hususan mafuta ya petrol na hivyo kuongeza gharama za uzalishaji. Kwa upande mwingine kupungua kwa thamani ya shilingi, kunaboresha ushindani wa bidhaa na huduma zetu tunazouza nje na kuongeza kipato cha Watanzania wanaouza bidhaa nje hususan wakulima wetu wa pamba, kahawa, korosho n.k. Changamoto yetu ni kuhakikisha kuwa wauzaji wa bidhaa nje wanaitumia vyema fursa kama hii, mara inapotokea, kwa kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa hizo.

26. Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kushuka kwa thamani ya shilingi, kunaongeza gharama za uzalishaji viwandani na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje. Kwa mfano, mafuta ya petroli na malighafi zinazotumika viwandani bei yake huongezeka thamani ya shilingi inaposhuka. Hata hivyo, kwa upande mwingine, kupungua kwa thamani ya shilingi kunaboresha ushindani wa bidhaa na huduma zetu tunazouza nje na hivyo kuongeza fursa ya ongezeko la pato la Taifa. Changamoto yetu ni kuhakikisha kuwa, tunazalisha na kuuza zaidi nje kuliko tunavyoagiza ili kunufaika na kushuka huko kwa thamani ya shilingi.

27. *Mheshimiwa Spika,* naomba kutoa ufafanuzi kuhusu fedha zilizopungua za kusaidia Bajeti (GBS) kutoka kwa wahisani katika mwaka 2010/11. Kupungua kwa misaada na mikopo ya kibajeti kunatokana na baadhi ya wafadhili kutoa fedha zilizokuwa zimepangwa kwa mwaka wa fedha 2010/11, kutolewa katika mwaka wa fedha wa 2009/10 ili kusaidia Serikali kupambana na athari za msukosuko wa kiuchumi duniani kama nilivyoeleza katika hotuba ya Bajeti. Hivyo ni dhahiri kuwa katika kipindi cha miaka miwili ya fedha 2009/10 na 2010/11 tutakuwa tumepata fedha zote za GBS kwa kipindi hicho kama ilivyotarajiwa. Aidha, kiasi cha shilingi 2,452.908 bilioni zinatarajiwa kupatikana kutokana na misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo.

28. *Mheshimiwa Spika,* baada ya kutoa maelezo kuhusu hoja zilizotolewa na Kamati ya Uchumi na Fedha, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nielezee kwa muhtasari mafanikio

ya Serikali ya Awamu ya Nne hadi sasa. Kama nilivyoeleza katika hotuba zangu mbili ya Hali ya Uchumi na ile ya Bajeti, Serikali ya Awamu ya Nne imepata mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali. Katika eneo la ukuaji wa uchumi kati ya mwaka 2005 na 2009, ukuaji wa uchumi umeendelea kuwa imara licha ya athari za msukosuko wa uchumi duniani, kupanda kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia na uhaba wa mvua uliotokea katika miaka ya 2005/06 na 2008/09. Katika kipindi hicho wastani wa ukuaji wa uchumi ulikuwa asilimia 6.9 kwa mwaka, kiwango ambacho kilikuwa ndani ya lengo la MKUKUTA la ukuaji wa uchumi wa kati ya asilimia 6 hadi 8 ifikapo mwaka 2010.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa na huduma nje yaliongezeka kutoka dola za kimarekani 2,948.3 milioni mwaka 2005 hadi kufika dola za kimarekani 4,693.6 milioni mwaka 2009. Aidha, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kutoka dola za kimarekani 2,048.4 milioni mwaka 2005, sawa na uwezo wa uagizaji bidhaa na huduma kwa miezi 4.8 na kufikia dola za kimarekani 3,551.3 milioni mwaka 2009, sawa uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma wa miezi 5.7.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2010 ni pamoja na:

(i) ukuaji wa pato halisi la Taifa kwa mwaka 2010 unatarajiwa kuwa asilimia 7 ukilinganisha na asilimia 6 ya mwaka 2009;

(ii) Juhudi za kukusanya mapato ya ndani (Revenue Efforts) inategemea kufikia uwiano wa pato la Taifa wa asilimia 17.3 mwaka 2010/11 ukilinganisha na asilimia 16.4 mwaka 2009/10;

(iii) Kasi ya upandaji bei inakadiriwa kupungua kufikia asilimia 8 mwezi Juni 2010 ukilinganisha na asilimia 10.7 mwezi Juni 2009. Aidha, kasi ya upandaji bei inategemewa kushuka zaidi na kufikia asilimia 5 ifikapo mwezi Juni 2011;

(iv) Hatua zitachukuliwa kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni za kutosha kukidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kwa kipindi kisichopungua miezi mitano (5).

31. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vilivyoainishwa katika Hotuba ya Hali ya Uchumi vimepangwa kulingana na maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi kwa haraka zaidi. Kilimo ikiwa ni pamoja na mifugo na uvuvi vimepewa uzito wa kipekee. Bajeti iliyotengwa na Serikali itasaidia katika kuwezesha maeneo yale ambayo sekta binafsi imekuwa ikikumbana na kikwazo katika kuwekeza. Hivyo, Bajeti hiyo ni mchango wa Serikali na mchango mwingine mkubwa unatoka kwa Sekta binafsi. Vipaumbele vingine ni miundombinu, uendelezaji wa ardhi na makazi, vitambulisho vya taifa, nishati, viwanda na sekta ya fedha.

32. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na vipaumbele vilivyoelezwa hapo juu napenda kutaja baadhi ya maeneo muhimu yaliyomo katika Bajeti ya 2010/11.

(i) Bajeti inalenga kufanikisha uchaguzi mkuu wa Oktoba 2010 kwa kutenga fedha za kuhakikisha uchaguzi mkuu unafanyika katika mazingira ya amani na utulivu;

(ii) Sekta ya elimu imetengewa shilingi 2,045.3 bilioni ikilinganishwa na shilingi 1,743.9 bilioni mwaka 2009/10 sawa na ongezeko la asilimia 17.2. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wote kuanzia elimu ya msingi hadi elimu ya juu ikijumuisha watoto wa masikini wanapata elimu. Serikali itaendelea kuboresha sekta ya elimu hatua kwa hatua kulingana na uwezo wake pamoja na michango ya sekta binafsi na asasi nyingine;

(iii) Bajeti imetenga fedha kwa ajili ya mchakato wa kutengeneza vitambulisho vya Taifa ili watanzania tutambuane. Vitambulisho vya Taifa vitasaidia kuwarahisishia wananchi kupata huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii;

(iv) Bajeti ya maji imeongezeka kwa asilimia 14.5 ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi mijini na vijijini. Hatua hii ni kwa manufaa ya jamii;

(v) Kuongeza bajeti ya kilimo ili kuimarisha huduma za ugani, kufanya tafiti katika uzalishaji wa mbegu na mifugo bora na kuongeza ruzuku za madawa na mbolea;

(vi) Kupanua na kukarabati miundombinu ya barabara, reli, na viwanja vya ndege, na hivyo kuongeza bajeti ya miundombinu kwa asilima 37.3. Sote tunakubaliana kuhusu umuhimu wa kuboresha na kupanua miundombinu;

(vii) Kuboresha sekta ya afya kwa kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na hospitali na ukarabati wa hospitali za Mikoa na ununuzi wa madawa kwa kuongeza bajeti kwa asilimia 25.2. Serikali inafahamu umuhimu wa kuboresha afya kwa jamii;

(viii) Kuboresha maslahi ya watumishi. Sote tunafahamu umuhimu wa kuboresha maslahi ya watumishi katika kuongeza ari, juhudi na ufanisi kazini;

(ix) Bajeti hii imelenga kuongeza mtaji wa Benki ya Wanawake nchini kwa shilingi bilioni mbili kila mwaka ili huduma zake ziwafikie wanawake wengi zaidi. Kuwawezesha wanawake katika shughuli zao kwa kuwapatia vyanzo vya mikopo nafuu ni jambo jema kwa jamii yote, kwani kina mama wanabeba jukumu zito katika familia;

(x) Kuanzisha dirisha la kilimo na kuanzisha Benki ya Kilimo ili kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wakiwemo wakulima wadogo wadogo. Hii ni hatua muhimu katika kutekeleza kaulimbiu ya kilimo kwanza; na

(xi) Kuboresha sekta ya fedha kwa kuanzisha Benki ya Kilimo, kuimarisha Benki ya Rasilimali, kuharakisha utekelezaji wa kutoa huduma ya kukodisha

zana za kilimo na ujenzi (Financial Leasing) na kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya fedha ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi juu ya uwekaji akiba katika mabenki.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya hatua kubwa zinazochukuliwa na Serikali ni kuboresha kilimo kupitia Bajeti hii na kuweka misingi na mazingira ya upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa Sekta hiyo. Ikumbukwe kuwa upatikanaji wa fedha za kugharamia kilimo ni moja ya nguzo kumi za Kilimo Kwanza na utekelezaji wake umepangwa kwa kuoanishwa na dira ya Taifa ya maendeleo 2025 pamoja na mpango wa kuendeleza Sekta ya kilimo.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na maelezo hayo hapo juu, ni dhahiri kuwa bajeti ya mwaka huu ni ya kipekee na ambayo inazingatia mahitaji ya wananchi katika ngazi mbalimbali ikiwemo wananchi wa vipato vidogo mijini na vijijini. Ni ukweli usiopingika kuwa kwa azma hii ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, CCM ina nafasi kubwa ya kuendelea kuongoza na kuwaletea Watanzania maisha bora.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti ya 2010/11 ni mwendelezo wa jitihada za Serikali katika kufikia malengo ya MKUKUTA, Malengo ya Maendeleo ya Milenia, na hatimaye Dira ya Maendeleo 2025. Hata hivyo, ili kufikia malengo yetu mapema zaidi, kila mwananchi anapaswa kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa zinazojitokeza kwa kuzalisha mali na kujiongezea kipato.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki katika uzalishaji kwa mwananchi mmoja mmoja au katika vikundi ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wetu. Aidha, sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda zikiboreshwa na kutilia mkazo usindikaji wa mazao ya kilimo, zina nafasi kubwa ya kuchangia Pato la Taifa na kukuza ajira. Bajeti hii pia inalenga kuongeza jitihada za Serikali za kuendeleza ardhi, na kuunganisha nchi yetu kwa njia ya miundombinu ya barabara, reli, mawasiliano na nishati.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya 2010/11 imeandaliwa katika mazingira magumu kufuatia msukosuko wa kiuchumi uliokumba nchi yetu na mabadiliko ya tabianchi iliyosababisha ukame na njaa katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Aidha, Bajeti hii imeandaliwa katika mazingira ambayo bei ya mafuta ya petroli imeendelea kuongezeka. Vile vile ni kipindi ambacho misaada na mikopo ya kibajeti imepungua ukilinganisha na mwaka unaomalizika wa 2009/10. Pamoja na changamoto hizo, Serikali imeweza kubuni vyanzo mbadala vya mapato ambavyo vimewezesha Serikali kuongeza mgao wa matumizi kwa Sekta za kilimo, miundombinu, elimu, afya na maji. Ni matumaini ya Serikali kwamba utekelezaji wa Bajeti hii utasaidia sana kusukuma maendeleo kwa kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti hii ni Bajeti rafiki na imemlenga mwananchi wa kawaida. Bajeti pia imetoa fursa kwa Sekta binafsi kupitia utaratibu wa PPP. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono

Bajeti hii ili kutimiza azma ya kuwaletea maendeleo wananchi hivyo kuboresha maisha yao.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine tena napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na kwa kunipa heshima ya kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa nusu ya pili ya kipindi cha kwanza cha Awamu ya Nne. Aidha, napenda kumshukuru Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais kwa uongozi wake na hasa katika kutatua kero za Muungano. Vile vile, namshukuru Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali Bungeni na kwa ushirikiano na maelekezo mbalimbali yaliyonisaidia kutekeleza kazi zangu kwa ufanisi. Namshukuru Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha Bunge letu kwa viwango vya hali ya juu wakati wote. Nawashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge, Mawaziri wenzangu na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano walionipa wakati wa kutekeleza majukumu yangu kama Waziri wa Fedha na Uchumi.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Wizara ya Fedha na Uchumi, napenda tena kuwashukuru Naibu Mawaziri, Mhe. Jeremia H. Sumari (Mb) na Mhe. Omari Y. Mzee (Mb). Namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Ramadhani M. Khijjah na Naibu Makatibu Wakuu, Ndugu John M. Haule, Ndugu Laston T. Msongole na Dkt Servacius B. Likwelile, pamoja na Katibu Mtendaji

Tume ya Mipango; Dkt. Philip. I. Mpango. Napenda kuwashukuru Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania Prof. Benno Ndulu, na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ndugu Harry Kitillya kwa ushirikiano walionipatia wakati wote nikiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Aidha, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kilosa kwa kunipa ridhaa ya kuwa Mbunge wao na kwamba naamini watanipa tena nafasi ya kuwawakilisha kwa kipindi kinachokuja.

Mheshimiwa Spika, **naomba kutoa hoja.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

MAELEZO YA NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI

MHE. OMAR YUSUF MZEE (MB)

AKIJIBU BAADHI YA HOJA ZA WAHESHIMIWA

WABUNGE KUHUSU HOTUBA YA HALI YA UCHUMI MWAKA 2009

NA BAJETI YA SERIKALI 2010/11

DODOMA

JUNI, 2010

42. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja mbili zilizowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mhe. Mustafa Haidi Mkulo (Mb.). Napenda kuunga mkono hoja zote mbili zilizoandaliwa kwa umahiri mkubwa na kwa kuzingatia masuala muhimu ya kitaifa na ambayo ni nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.

43. ***Mheshimiwa Spika***, Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuongoza kwa hekima katika kipindi cha kwanza cha awamu hii. Aidha, napenda kuwashukuru Mhe. Dkt. Abdallah Omari Kigoda (Mb - Handeni), Mhe. Hamad Rashid Mohamed (Mb - Wawi) na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba hizi. Vile vile, napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa Kiembe Samaki, kwa kunichagua kuwa mbunge na mwakilishi wao bungeni. Naamini wameridhishwa na kazi nzuri niliyoifanya katika kuleta maendeleo jimboni na Taifa letu kwa ujumla.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili hotuba ya bajeti kwa mwaka wa 2009/10 kama ifuatavyo:-

45. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu idadi ya watu, ushauri umepokelewa. Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 2006 inasisitiza umuhimu wa kuwa na uwiano mzuri wa idadi ya watu na ukuaji wa uchumi. Mkakati wa

Serikali katika kutekeleza Sera hiyo imekuwa pamoja na kutilia mkazo elimu ya Sekondari hasa kwa wasichana, kuongeza uzalishaji hasa katika kilimo, na kutoa elimu ya uzazi kwa Umma. Hata hivyo, Serikali inapenda kutoa wito kwa kila Mtanzania kutambua kwamba kuongezeka haraka kwa idadi ya watu katika familia ni mzigo mzito kwa familia yenyewe na Taifa kwa ujumla kwa maana ya uwezo wa kumpatia kila mmoja mahitaji yote ya msingi.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kueleweka vizuri kwa wananchi, ushauri huo utazingatiwa. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 imekuwa ikitekelezwa kupitia mipango na mikakati mbalimbali kama vile, MKUKUTA na mipango mingine ya kisekta. Mwaka 2009 Serikali kwa kutumia mtaalam elekezi ilifanya mapitio ya utekelezaji wa Dira. Kazi hiyo ilibaini mapungufu mbalimbali katika utekelezaji wa Dira. Kufuatia kuundwa upya kwa tume ya Mipango, Serikali imeazimia kuzifanyia kazi changamoto zote zilizobainika na kuchukua hatua zinazofaa, ikiwa pamoja na kurejea mfumo wa utayarishaji wa mipango ya maendeleo ya miaka mitano-mitano ili kutoa fursa nzuri zaidi ya kupima utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mpango wa kwanza (2011/12-2015/16) unatarajiwa kuzinduliwa mwaka ujao wa fedha. Vile vile, Tume ya Mipango inaandaa utaratibu na mbinu mpya za kuitangaza Dira ili ieleweke vizuri na kumwezesha kila mwananchi kutambua wajibu wake katika kuitekeleza Dira.

47. HOJA: *Serikali kukopa kutoka vyanzo vya ndani itafifiza sekta binafsi na kusababisha viwango vya riba kupanda*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali inatarajia kukopa shilingi 1,331.2 bilioni kutoka soko la ndani na nje kwa lengo la kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, hususan, miradi ya miundombinu. Kutokana na benki za biashara kuendelea kuchukua tahadhari katika kutoa mikopo kwa sekta binafsi kutokana na msukosuko wa fedha duniani, benki nyingi zimeendelea kuwa na fedha nyingi. Hivyo, Serikali inaona ni busara kukopa fedha hizo kwa ajili ya bajeti yake ya maendeleo. Kwa hiyo, uamuzi huo wa Serikali kukopa hautarajiwi kuathiri uwezo wa benki hizo kukopesha sekta binafsi. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba kuna viwango vya ukwasi vinavyowiana na shughuli za kiuchumi kwa lengo la kutoathiri mikopo kwa sekta binafsi na kuleta utulivu katika viwango vya riba.

48. HOJA: *Hadi leo hakuna tathimini rasmi ya MKUKUTA I hivyo tunaingia MKUKUTA II na kasoro za MKUKUTA I.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Si kweli kwamba tathmini ya MKUKUTA I haikufanyika. Tathmini nyingi zilifanyika kutathmini utekelezaji wa MKUKUTA I kama sehemu muhimu katika mchakato wa maandalizi ya MKUKUTA II. Utekelezaji wa MKUKUTA I umewezesha kupata mafanikio katika sekta ya maji, elimu na afya na taarifa za utekelezaji zinapatikana katika maandiko mengi, ikiwa ni pamoja na Taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa MKUKUTA (MAIR), taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu (PHDR). Aidha, napenda kueleza kuwa, MKUKUTA II unatokana na uchambuzi wa utekelezaji wa MKUKUTA I ikibainisha mafanikio,

changamoto, na matarajio yanayotokana na utekelezaji wa MKUKUTA I. Aidha, warsha za kikanda zilifanyika nchi nzima zilizotoa fursa kwa wadau mbalimbali kuchangia maoni yao kuhusu utekelezaji wa MKUKUTA I na mapendekezo ya maandalizi ya MKUKUTA II. Kwa maelezo hayo, ni dhahiri kuwa tunaingia katika kutekeleza MKUKUTA II tukiwa na taarifa zote muhimu za mafanikio, changamoto za utekelezaji wa MKUKUTA I na matarajio ya MKUKUTA II.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA II unalenga maeneo machache yanayogusa watu wengi zaidi na yanayotekelezeka. Aidha makisio ya ugharamiaji wa MKUKUTA II utafanyika hasa kwa kuzingatia programu na miradi itakayotuwezesha kufikia malengo ya MKUKUTA II na mapitio ya mara kwa mara yatafanyika.

49. HOJA: *Wakulima waelimishwe kuhusu upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wadogo wadogo na Serikali itenge fedha kwa ajili hiyo;*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** kulingana na Mwongozo wa Ukopeshaji (lending framework) wa Dirisha la Kilimo ulioidhinishwa na Serikali na ambao TIB inautumia, Makampuni makubwa yametengewa asilimia 35 tu ya fedha zote za Mfuko. Kati ya fedha zilizobakia, asilimia 30 ni kwa ajili ya taasisi za kutoa mikopo midogo midogo (zikiwemo benki za kijamii, Microfinance Institutions -MFIs,), wakati asilimia 30 nyingine zimetengwa kwa ajili ya Vyama vya Ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS), vikundi vya wakulima wadogo wadogo vilivyosajiliwa, n.k. Asilimia 5 iliyobaki ni ya kugharamia ushauri na mafunzo kwa wakulima wadogo kuhusu jinsi ya

kuweza kunufaika na Dirisha la Kilimo. Inatarajiwa pia kuwa, wakopaji wa jumla kama benki za kijamii, MFIs, SACCOs, n.k. watawaelimisha wakulima wadogo ambao ni wakopaji wao watarajiwa.

50. HOJA: *Dhahabu inachangia asilimia 40.9 ya mapato yatokanayo na mauzo nje. Mapato kutokana na mauzo ya dhahabu ni kiasi gani kwa mwaka?*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** ni kweli kabisa kuwa dhahabu ndiyo inayochangia kiasi kikubwa katika mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje. Mauzo ya dhahabu nje yaliongezeka kwa asilimia 15.4 kutoka dola za kimarekani milioni 932.4 mwaka 2008 hadi dola za kimarekani milioni 1,076.1 mwaka 2009.

51. Hoja: *Usimamizi wa Matumizi ya fedha za Umma uende sambamba na kutoa adhabu kali kwa wale wote wanaofuja rasilimali za Taifa.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Fedha na Uchumi ipo katika mchakato wa kufanya marekekebisho ya Sheria ya fedha za Umma sura 348 ili kuimarisha usimamizi wa fedha za umma ikiwa ni pamoja na kuweka adhabu kali kwa wale wote watakaobainika kufuja rasilimali za Taifa. Aidha, sheria ya mkaguzi mkuu wa mahesabu (CAG) inarekebishwa ili kumpa mkaguzi mkuu wa mahesabu uwezo wa kuchukua hatua ya kuwasiliana na vyombo vya uchunguzi endapo atabaini kuwa upotevu wa mali za umma usio na maelezo ya kumridhisha.

52. HOJA: *Uwiano wa matumizi ya maendeleo umezidi kushuka dhidi ya matumizi ya kawaida*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Kama inavyoonekana kwenye Hotuba ya Bajeti 2010/11, Jedwali Na. 2a na 2b; Matumizi ya maendeleo kama asilimia ya Pato la Taifa yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, matumizi halisi ya maendeleo yaliongezeka kutoka asilimia 7.9 ya Pato la Taifa mwaka 2007/08 hadi asilimia 9.1 mwaka 2009/10 na inatarajiwa kuwa asilimia 11.0 mwaka 2010/11. Hata hivyo, matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha malipo ya madeni, pensheni, mishahara na matumizi mengineyo ya uendeshaji wa Serikali yameendelea kukua kwa kiwango kikubwa zaidi. Ningependa kumjulisha Mhe. Mbunge kuwa, ukuaji wa matumizi ya maendeleo huchangia kuongezeka kwa matumizi ya kawaida sababu miradi ikikamilika inahitaji fedha za uendeshaji. Kwa mfano, ujenzi wa shule ambao ni matumizi ya maendeleo huchangia kupanuka kwa mahitaji ya matumizi ya kawaida kwa maana ya mahitaji ya walimu zaidi, vitabu na gharama nyingine za uendeshaji.

53. HOJA: *Kuwe na mfumo unaoongoza na kupanua wigo wa kodi*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mapato katika mpango wake wa miaka mitano imejipanga kuongeza mapato ya Serikali mwaka hadi mwaka. Mbinu mojawapo inayozingatiwa ili kutimiza azma hiyo ni kupanua wigo wa kodi. Mamlaka ya Mapato imejiwekea lengo la kusajili walipakodi wapya kwa ongezeko la kiwango cha asilimia ishirini (20%) kwa mwaka. Aidha, hatua zinazochukuliwa na mradi wa MKURABITA wa kurasimisha

biashara za sekta isiyo rasmi pamoja na hatua za kutengeneza vitambulisho vya Taifa vitasaidia kupanua wigo wa kodi.

54. HOJA: *Serikali iibue vyanzo vipya vya mapato kama vile nyumba za kupanga, maduka ya biashara na viwanja na kodi inayotokana na uharibifu wa mazingira.*

JIBU*:* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa inapata mapato stahili kutoka kwenye vianzio hivyo kwa kutumia utaratibu wa kukusanya kodi kwa njia ya vitalu na kufanya uthamini wa majengo na mali nyingine zisizo hamishika.

Nyumba za kupanga na vyumba vya maduka vinatozwa kodi ya mapato kwenye pango "rental tax", kodi ya ongezeko la thamani kama kiasi cha pango kwa mwaka kinafikia shilingi milioni 40, na kodi ya majengo "property rate" ambayo inakusanywa na Serikali za Mitaa. Pia tunapenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa wamiliki wa viwanja wanatozwa kodi ya viwanja "land rent".

Kuhusu suala la kuanzisha kodi ya mazingira, Serikali inakubalina na Mheshimiwa Mbunge hivyo italifanyia uchambuzi wa kina na kuona jinsi gani itatoza kodi hiyo.

55. HOJA: *Pamoja na kupunguza ushuru katika kilimo na mifugo wakulima hawajawezeshwa katika masuala ya kulima na kusafirisha mazao*

Jibu: ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekuwa ikikipa kilimo msukumo wa pekee, pamoja na juhudi nyingine, kwa kupunguza au kuondoa kabisa kodi mbalimbali katika pembejeo za kilimo. Hatua hizo zimetekelezwa hatua kwa hatua ili kutoathiri mapato ya Serikali. Ikumbukwe pia, pamoja na Serikali kupunguza na kusamehe kodi katika kilimo, Serikali pia inatoa ruzuku za pembejeo za kilimo.

56. HOJA: *Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri wasimamiwe na Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, Kama vile wale wa Serikali Kuu.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti, katika marekebisho ya sheria ya fedha itakayoletwa katika Bunge hili, Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani itakayoanzishwa chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, itasimamia Wakaguzi wa Ndani wote ikiwa ni wale wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

57. HOJA: *Kitabu cha Mapato-kitabu cha kwanza, (Volume 1-Financial Statement and Revenue Estimates), hakionyeshi Mapato ya Ubinafsishaji (Privatisation Proceeds).*

58. JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Mapato ya Ubinafsishaji ya shilingi bilioni 30, yameonyeshwa kwenye kitabu cha kwanza "Kitabu cha Makadirio ya Mapato". Katika Jedwali la 1, Ukurasa wa kumi (x) – (Summary of Recurrent Revenue Estimates 2010/11).

59. HOJA*:* *Ni lini Mamlaka ya Mapato itakuwa na majengo huko Mtambaswala*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** tayari suala hili linashughulikiwa na Wizara ya Miundombinu kwa maana ya kujenga ofisi za kudumu zitazokidhi mahitaji ya idara zote za Serikali (TRA, Uhamiaji na Polisi). Hata hivyo, kwa hivi sasa maofisa wa Mamlaka ya Mapato wamekwisha pelekwa kwenye mpaka wa Tanzania na Msumbiji kwenye Daraja la Umoja huko Mtambaswala na wanatumia kwa pamoja ofisi na maofisa wa uhamiaji kwenye majengo yaliyokuwa yanatumiwa na Mkandarasi wa ujenzi wa daraja hilo.

60. HOJA: *Halmashauri kubakiwa na fedha nyingi mwisho wa mwaka tatizo ni nini?*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Halmashauri hupokea fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali vya ndani na nje ambapo shughuli zote hutekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi mwisho wa mwaka, Halmashauri zimekuwa zikibakiwa na fedha nyingi kwenye akaunti zake zikijumuisha fedha za mapato kutokana na vyanzo vyao, fedha za ruzuku ya maendeleo kutoka Serikali Kuu, miradi ya moja kwa moja ya wahisani. Miongoni mwa sababu zinazopelekea kubakiwa na fedha nyingi ni pamoja na:

a. Uwezo mdogo wa Halmashauri wa kutumia fedha hizo kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazotakiwa kufuatwa;

b. Halmashauri kuwa na akaunti nyingi katika ngazi ya wilaya, kata na vijiji ambazo hazina utaratibu mzuri wa kutumia fedha kwa wakati;
c. Kuchelewa kubadilishana taarifa za upokeaji wa fedha miongoni mwa wakuu wa idara za Halmashauri, na kutokuwa na mazoea ya kusoma taarifa za migao ya fedha kwenye tovuti ya Hazina (www.mof.go.tz);
d. Mchakato wa ununuzi kuchelewa kuanza kutekelezwa huku wakisubiri upokeaji wa fedha;
e. Baadhi ya fedha hasa za nje kuchelewa kupokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;
f. Kuchelewa kurudisha Hazina mishahara isiyolipwa (Unclaimed salaries); na
g. Kuchelewa kuwasilisha makato ya wafanyakazi ya kisheria kwenye mifuko mbalimbali ya hifadhi za jamii au taasisi za kifedha.

Hata hivyo, kama nilivyoeleza kwenye Hotuba yangu, Halmashauri zinatakiwa kuonesha bakaa katika akaunti zao ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha ili zijumuishwe kwenye bajeti ya mwaka unaofuata kama chanzo cha mapato.

61. HOJA: *Bakaa ya mfuko wa jimbo zimetumwa lini kwenye majimbo husika?*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa Fedha 2009/10, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 10.0 bilioni kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Serikali ilitoa fedha za awamu ya kwanza mwezi April, 2010 (shilingi 5.0 bilioni). Pia Serikali imetoa fedha za awamu ya mwisho za mfuko huo (Shilingi 5.0 bilioni) mwanzoni mwa mwezi Juni, 2010.

62. HOJA: *Serikali imeendelea kuwa na Watumishi hewa (Ghost Workers), kwa nini inashindwa kudhibiti matumizi yake?*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaongeza juhudi katika kuhakikisha watumishi hewa wanafutwa kwenye 'Payroll'. Vile vile, Maafisa Masuuli wote wameelekezwa kuhakiki orodha ya watumishi wao kabla ya malipo. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilifanya uhakiki wa mishahara kwenye Mikoa 10 ikijumuisha Halmashauri 58 za mikoa hiyo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2010/11, Serikali imeanzisha Fomu maalum ili kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa watumishi waliofariki, walioacha ama walioachishwa kazi, waliostaafu, na watumishi waliopo kwenye likizo bila malipo. Fomu hiyo pia inatumika wakati wa bajeti kuonesha watumishi watakaostaafu katika mwaka wa fedha unaofuata. Vile vile, Serikali imepanga kufanya ukaguzi wa kina wa mishahara katika mafungu yote.

Katika kudhibiti matumizi, Serikali itaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu wa matumizi yake yote (matumizi ya kawaida na maendeleo) ili

kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kama ilivyokusudiwa. Katika kufanikisha hili, Serikali itatumia kitengo vya ufuatiliaji matumizi (Expenditure Tracking) na kitengo kinachofuatilia matumizi kwenye miradi (Technical Audit)

63. HOJA: *Bajeti ya sekta ya Mahakama iongezwe.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuongeza fedha mwaka hadi mwaka katika sekta ya mahakama ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki zao kwa wakati. Serikali imeendelea kuongeza fedha ili kuharakisha uendeshaji wa kesi pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi. Katika mwaka wa fedha 2010/11 Sekta ya Mahakama imetengewa jumla ya shilingi 139.4 bilioni ikilinganishwa na shilingi 103.4 bilioni mwaka 2009/10.

64. Hoja: *Benki ya Kilimo itoe mikopo kupitia SACCOS na riba iwe nafuu.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Benki ya Kilimo ipo njiani kuanzishwa. Hata hivyo, kwa hivi sasa dirisha la kilimo limeanzishwa ndani ya TIB. Dirisha hilo linatoa mikopo kwa wakulima kupitia SACCOS kwa riba ya asilimia 8 ambayo ni nafuu ikilinganishwa na benki nyingine ambazo zinatoza riba zaidi ya asilimia 15.

65. HOJA: *Katika zoezi la sensa ya watu na makazi, Serikali itenge rasilimali ya kutosha ili kuwabaini watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali ndani ya familia.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulielezea Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mara ya kwanza takwimu za watu wenye ulemavu zilianza kupatikana katika sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2002 ambapo matokeo yalionesha kuwa asilimia 2 ni watu walemavu. Aidha, sensa ijayo inatarajiwa kufanyika mwaka 2012 na itakuwa ni sensa ya kipekee ikilinganishwa na sensa zilizopita kwani inakusudia kuongeza moduli ambazo itaipatia nchi yetu viashiria mbalimbali vitakavyojumuisha watu katika rika mbalimbali la umri, hali ya ndoa, uraia, ulemavu, uzazi na vifo, hali ya makazi na umilikaji wa rasilimali katika kaya. Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya zoezi hilo kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita na itaendelea kufanya hivyo hadi wakati wa sense hiyo.

66. HOJA: *Katika utaratibu wa Cash Budgeting kumekuwa na ulimbikizaji wa madeni na mihadi inayofikia shilingi 500 bilioni, wahusika wachukuliwe hatua.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inachukua hatua mbalimbali ili kudhibiti ulimbikizaji wa madeni na mihadi. Katika mwaka 2010/11, Serikali inadhamiria kuanza kutumia mfumo wa malipo kabla ya huduma za umeme na simu (kama Luku) kwa Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mikoa. Hatua hii pamoja na kusaidia Serikali kudhibiti ulimbikizaji wa

madeni, itaimarisha Kampuni za simu na umeme (TTCL na TANESCO) kimapato.

Aidha, Serikali inasisitiza kuzingatia Sheria ya Fedha na Sheria ya Ununuzi wa Umma ipasavyo, pamoja na kutumia mfumo wa Malipo ya Serikali. Utaratibu huu unamlazimisha Afisa Masuuli kutopata huduma bila ya kuwa na fedha, hivyo utadhibiti malimbikizo ya madeni kwa kuwa watoaji huduma Serikalini watakuwa na uhakika wa malipo yao.

67. HOJA: *Compliant Trader katika ulipaji wa ushuru wa forodha wasimamiwe vema ili kujua wazuri na wabaya*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2007, Mamlaka ya Mapato ilianzisha mpango wa "Compliant Traders" kwa lengo la kuwarahisishia utoaji mizigo bandarini. Ili kuweza kuingia kwenye mpango huu, Mamlaka imeweka vigezo maalum ikiwa ni pamoja na kuthibitisha kuwa waingizaji bidhaa hao ni compliant kwa sheria zote za mamlaka na Idara nyingine za Serikali (OGDS). Baada ya kuingia kwenye utaratibu huu, "Compliant Traders" hufanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara ndani ya kila robo mwaka kujiridhisha na utimizaji wao wa wajibu wa masharti yaliyowekwa. Orodha nzima hupitiwa kila mwezi na kufanya tathmini. Mpango ulianza na wafanyabiashara 54 mnamo mwaka 2007. Kufuatia uhakiki na ukaguzi nilioutaja hapo juu, watatu (3) waliondolewa kwa kukiuka masharti na wapya wawili wamesajiliwa mwaka huu 2009 – 2010 na kufikia idadi ya 53 mpaka kufikia Mei, 2010.

68. HOJA: *Hatua gani Serikali imechukuwa kulipa malimbikizo ya madeni na madai ya makandarasi ya Wizara ya Miundombinu ambayo yamefikia kiasi cha shilingi 259,255,651,327 kwa mchanganuo ufuatao:-*

i) Hati za madai ya makandarasi Shilingi 48,015,081,327/=

ii) Malipo ya awali (advance) Shilingi 135,983,000,000/=

iii) Fidia miradi ya barabara - Shilingi 75,257,570,000/=

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kushughulikia madeni na madai yaliyopo, hadi kufikia tarehe 9 Juni, 2010, Serikali imelipa albaki ya hati za madeni yenye jumla ya shilingi 36 bilioni kwa hati (Certificates) zote zilizowasilishwa Hazina na hivyo kuweza kulipa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge mwaka 2009/2010. Aidha, italipa sehemu ya madeni kiasi cha shilingi 100 bilioni kabla ya mwisho wa mwezi huu kwa utaratibu wa uhamisho. Kadhalika, madeni na madai yaliyobakia ya shilingi 123.8 bilioni ambazo hazipo katika bajeti ya mwaka 2009/2010, yatalipwa mwaka ujao wa fedha. Madai haya ni ya kazi zinazoendelea kwenye miradi husika. Vile vile, Wizara ya Miundombinu itapitia mpango wake na bajeti ili kuainisha mahitaji halisi ya kutosheleza kazi za barabara zilizopangwa kutekelezwa ndani ya mwaka mmoja wa 2010/11. Kwa mfano, fidia kwa watu watakaoathiriwa kwa kupisha ujenzi wa barabara itabidi ifanyike tu kwa sehemu ya barabara itakayojengwa ndani ya mwaka mmoja.

69. HOJA: *Serikali iweke utaratibu wa kutuma kwenye Halmashauri fedha zote kwa wakati mmoja ili kurekebisha matatizo ya ucheleweshwaji wa fedha uliopo hivi sasa.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Kulingana na utaratibu wa kutumia kile kinachokusanywa (Cash Budget) kwa kila mwezi, siyo rahisi kuzipelekea Halmashauri fedha zote kwa mara moja na hasa ikizingatiwa kuwa kuna mambo mengi ya kitaifa ambayo pia hutegemea fedha hizo zinazokusanywa kila mwezi. Aidha, mbali na mahitaji ya Kitaifa, tunazo pia Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa ambazo pia zina shughuli muhimu za kutekeleza na hutegemea makusanyo hayo hayo ya kila mwezi.

70. HOJA: *Serikali ifanye tathmini ya kina ili kubaini hatua sahihi zitakazosaidia kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri nchini.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Matumizi mabaya ya fedha za umma kwa baadhi ya Halmashauri yanatokana na kutozingatia sheria na kanuni za fedha. Wizara ya Fedha na Uchumi inaendelea kuwapa mafunzo ya mara kwa mara wafanyakazi wa Serikali za Mitaa kuhusu taratibu za matumizi ya fedha za umma na kuimarisha vitengo vya mipango, uhasibu na ukaguzi wa ndani kwa kuajiri watumishi wapya.

71. Hoja: *Kuna urasimu sana Benki ya Rasilimali Tanzania(TIB) ambapo tangu mwaka jana na licha ya kupewa shilingi 19 bilioni, mikopo ya matrekta kwa SACCOS za Morogoro haijatolewa.*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika***, ni kweli kuna baadhi ya SACCOS za Morogoro zilileta maombi ya mikopo TIB tangu mwaka jana lakini kwa

wakati huo mwongozo wa ukopeshaji haukuwa tayari na fedha zilikuwa bado kuidhinishwa na Bunge na kutolewa kwa TIB. Mwongozo huo umekamilika Desemba 2009, na idhini ya Bunge ilitolewa Februari 2010. Baada ya idhini hiyo, mchakato wa kutathmini mikopo ya dirisha la kilimo ulianza na wakati huo SACCOS za Morogoro ziliingia mkataba na "Private Agricultural Support Services (PASS)" kwa ajili ya kuandaa Business Plan. Baadhi ya Business Plan hizo zimekamilika mwezi huu wa Juni 2010 na hivyo mikopo kwa SACCOS hizo itaanza kutolewa hivi karibuni. Aidha, TIB ilikishapokea shilingi 19 bilioni kufikia mwishoni mwa Machi 2010 kwa ajili ya Dirisha la Kilimo.

72. Hoja: *Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imekusanya kodi kiasi gani kutoka kwenye sukari ya magendo inayokamatwa huko Kyela*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa uingizaji wa sukari huhitaji kibali kutoka Bodi ya Sukari, Mamlaka ya Mapato Tanzania hukamata na kutaifisha sukari yote inayoingizwa bila ya vibali. Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2009 mpaka Mei 2010, kiasi cha kilo 31,520 zilikamatwa na kutaifishwa. Kiasi hiki kiliuzwa kwa taasisi za umma kama magereza, shule na vyuo kwa bei ya shilingi 850 kwa kilo na kuiingizia Serikali shilingi 26,792,000.

73. HOJA: *Sera za kodi zinaua Viwanda, Saruji inaingizwa kutoka nje ambayo imepata ruzuku*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** hivi sasa ushuru wa forodha wa asilimia 25 hutozwa kwenye saruji inayoagizwa kutoka nje. Aidha, kiwango hiki cha ushuru kilizingatia hali ya uzalishaji wa bidhaa hiyo katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mwaka 2007/08, ushuru wa forodha kwa saruji inayoagizwa kutoka nje ulipunguzwa kutoka asilimia 35 hadi asilimia 25, kutokana na uhaba wa bidhaa hiyo katika soko la ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile, Nchi za Jumuiya zilikubaliana kupunguza ushuru ili kuwawezesha wananchi kupata saruji kwa bei nafuu.

Kama nilivyoieleza kwenye hotuba yangu, tarehe 12 mwezi Mei, 2010, Mawaziri wa Fedha wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walijadili mapendekezo ya Nchi hizo ya kufanya marekebisho ya viwango vya ushuru wa forodha wa saruji na walikubaliana kwamba ifanyike tathmini mahsusi ili kujua viwango vya uzalishaji, mahitaji na bei ya saruji katika soko la Jumuiya ili waweze kufanya uamuzi sahihi ya kiwango chenye kuleta tija kwa wazalishaji na walaji wa bidhaa hiyo. Tathmini hiyo inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Desemba, 2010.

74. HOJA: *Malipo ya asilimia tano (5%) ya makusanyo yote ya kodi kwa wafanyakazi wa mamlaka ya mapato*

JIBU: ***Mheshimiwa Spika,*** Malipo yote ya kodi yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato kwa mujibu wa sheria za kodi husika na kwa nguvu

ya Sheria ya Mamlaka ya mwaka 1995 Sura ya 399 ya Sheria za Tanzania . Mamlaka ya Mapato hawapati malipo yoyote kwa uwiano wa asilimia ya kodi wanazokusanya na hivyo basi, wafanyakazi wa Mamlaka hawajawai kupata malipo ya asilimia tano ya makusanyo ya kodi.

Kila mwaka Mamlaka inawasilisha maombi yake ya matumizi kwa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa ajili ya kuendesha shughuli zake kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya Mamlaka ya Mapato.

***Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja.*